

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM



TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI UFADHILI WA MASOMO YA M.A. KISWAHILI

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) kwa kushirikiana na **Kampuni ya ALAF Limited** inafurahi kuwatangaza ufadhili wa ada kwa wanafunzi **watatu (3)** waliochaguliwa kusoma **Programu ya M.A. Kiswahili** katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa Mwaka wa Masomo 2021/2022.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

1. Awe raia wa Tanzania,
2. Awe mhitimu wa B.A. Kiswahili,
3. Awe na WAKIA (GPA) usiopungua 3.8 wa Digrii ya Kwanza,
4. Awe amepata udahili katika Programu ya M.A. Kiswahili ya CKD,
5. Awe na umri usiozidi miaka 30 wakati analeta maombi,
6. Awe mhitaji wa ufadhili wa ada,
7. Awe na uwezo wa kujigharimia mahitaji mengine (chakula, steshenari, malazi, utafiti n.k.).

Nyaraka Muhimu za Kutuma:

1. Barua ya maombi ambayo pia itabainisha uwezo wa kitaaluma,
2. Nakala ya cheti cha matokeo ya kitaaluma ya Shahada ya Kwanza (Transcript),
3. Nakala ya cheti cha kuzaliwa,
4. Maelezo mafupi (ukurasa mmoja) yanayobainisha sababu za kuhitaji ufadhili wa ada.

Maombi yatumwe kwa:

Mkurugenzi,

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Baruapepe: iks@udsm.ac.tz

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15/10/2021